

## Maswali na Majibu

1. Danieli aliweza kuambia Nebukadreza ndoto na maana yake namna gani?  
*Mungu alimwonyesha hiyo ndoto na maana yake.*
2. Mfalme Nebukadreza aliota nini?  
*Aliona sanamu kubwa iliyotengenezwa kwa madini tofauti – kichwa cha dhahabu, kifua na mikono ya fedha, tumbo na kiuno ya shaba, miguu ya chuma na nyayo za miguu ya chuma na udongo. Jiwe lilipiga hiyo sanamu ikaivunja kabisa na kuwa mlima.*
3. Ndoto ilikuwa na maana gani?  
*Mataifa yaliyotawala Mashariki ya Kati – dhahabu ni Babeli, fedha ni Wamedi na Wajemi, shaba ni Yunani, chuma ni Rumi, chuma na udongo ni taifa dhaifu na ya nguvu, jiwe ni Yesu anasimamisha Ufalme wa Mungu milele.*
4. Huu unabii utatimizwa lini?  
*Wakati Yesu atakuja kusimamisha Ufalme wa Mungu.*
5. Ezekieli aliona nini katika maono yake?  
*Bonde la mifupa mikavu iliyounganishwa pamoja. Nyama zikakua juu yake, zikapumua na kusimama kama jeshi kubwa.*
6. Huu unabii ulimaanisha nini?  
*Wayahudi walitawanyika dunia mzima, lakini hatimae watarudi kwa nchi yao na kuwa taifa tena.*
7. Wayahudi walitawanyika kwa mataifa ya dunia lini?  
*Mwaka wa 70 baada ya Yesu, wakati Warumi waliharibu Yerusalem.*
8. Wayahudi wamekuwa nje ya nchi yao kwa karibu muda gani?  
*Karibu miaka elfu mbili.*
9. Taifa la Israeli lilisimamishwa tena kwa nchi yao lini? *Mwaka wa 1948.*
10. Danieli na Ezekieli walijuaje kitakachokuwa kwa wakati ujao?  
*Mungu anajua kila kitu. Mungu aliwaonyesha kitakachokweko baadaye.*

## Mistari ya kukariri

Danieli 2:44      Ezekiel 37:14      Matendo 3:20 – 21

## Mazungumzo

Zungumza juu ya maono ya Ezekieli. Mbona Wayahudi walitawanyika na lini? Huu unabii ultimizwa namna gani juzijuzi?

## Kuandika

Chora sanamu yenye Nebukadreza aliona. Onyesha madini iliyokuweko na mataifa iliyosimamia.

## Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



### Somo la 29 Unabii juu ya wakati ujao

**SOMA** Danieli 2:1 – 5 na 27 – 45; Ezekieli 37:1 – 14

#### SOMO


Ingawaje Wayahudi walirudi kwa nchi yao, lakini hawakuwa na mfalme wao. Vile Mungu alikuwa amesema, wafalme wa khabila zingine waliwatawala. Wakati Danieli na Ezekieli walikuwa bado matekani, Mungu aliwapa unabii wa mambo yatakayofanyika kwa taifa lao na kwa mataifa ya watu wengine kwa wakati ujao. Huu unabii ulikuwa wakutia Wayahudi moyo kule utumwani.

Huu unabii wenye Mungu aliwapa Danieli na Ezekieli ulizungumzia mambo yatakayokuweko baada ya miaka nyingi. Hata mpaka wakati wetu wa sasa bado unatimizwa.

Danieli alichukuliwa na Mfalme Nebukadreza kama mtumwa mpaka Babeli. Alikuwa mmoja wa watu wa hekima wa Nebukadreza. Usiku mmoja Nebukadreza aliota ndoto ya ajabu iliyomtisha sana. Lakini ilipofika asubuhi alikuwa amesahau ndoto yenyewe. Alitaka watu wake wa hekima wamwambie maana yake. Watu wake wa hekima waliposhindwa kumwambia, Nebukadreza aliwatisha akitaka kuwaua wote.

Danieli aliomba Mungu na Mungu akamwonyesha ndoto na maana yake. Nebukadreza alikuwa ameona sanamu kubwa iliyotengenezwa kwa madini tofauti tofauti. Kichwa kilikuwa cha dhahabu, mikono na kifua vilikuwa vya fedha, tumbo na kiuno vilikuwa za shaba, miguu ilikuwa ya chuma na nyayo zi miguu ilikuwa nusu ya chuma nusu ya udongo.

Baadaye Nebukadreza aliona jiwe lililochogwa bila mikono. Hilo jiwe lilipiga hiyo nyayo ya miguu halafu sanamu ikaanguka na kuvunjika kwa vibande vidogo vidogo. Hilo jiwe likakua na kuwa mlima mkubwa uliojaza dunia yote.



Danieli alielezea Nebukadreza kwamba Mungu alikuwa anamwonyesha falme zitakazofuata baada ya ufalme wa Babeli. Kila madini kwa hiyo sanamu ilisimamia ufalme tofauti.

Kichwa cha dhahabu kilisimamia ufalme wa Babeli uliotawaliwa na Nebukadreza. Dhahabu ilikuwa madini mazuri ya kusimamia Babeli. Ilikuwa taifa ya utajiri mwingu. Madhabahu yote ilikuwa ya dhahabu ya kudumu.

Kifua na mikono ilikuwa ya fedha na ilisimamia taifa ya Wamedi na Uajemi. Mikono miwili ilionyesha mataifa mawili. Pesa ya hii taifa ilitengenezwa kutoka kwa fedha. Tumbo na kiuno ilikuwa taifa la Yunani. Wayunani walivaa silaha za shaba. Miguu ilikuwa ya chuma na ilisimamia taifa la Kirumi iliyokuwa na nguvu kama chuma.

Nyayo ya miguu ilikuwa ya chuma na udongo isiyochanganyikana. Hakujakuwa na taifa lingine la nguvu katika Mashariki ya Kati tangu utawala wa Kirumi. Kuna mataifa mengi yamekuweko, mengine ya nguvu kama chuma mengine dhaifu kama udongo. Hii inasimamia hali ya sasa.


Mataifa haya yalitawala Wayahudi kwa karne nyingi lakini walikuwa wanaishi kwa nchi yao. Hii ndoto ilionyesha ni taifa gani litawatawala Wayahudi mpaka aje mfalme wao wa haki – Yesu atakuja vile Mungu aliahidi.

Jiwe lilo chongwa kutoka mlimani bila mkono wa mtu linasimamia Yesu. Yesu alizaliwa bila baba wa kibinadamu. Wakati wa utawala wa nguvu na utawala dhaifu, Mungu atatuma Mwanawe, Yesu (jiwe) kuja kuharibu ufalme wa watu. Halafu Yesu atasimamisha Ufalme wa Mungu Israeli. Ufalme wa Mungu utakua mpaka ujaze dunia yote na kudumu milele.

Ezekieli pia alikuwa na maono kutoka kwa Mungu, akimwonyesha nini ingefanyika kwa taifa lake la Wayahudi kwa wakati ujao. Wayahudi walikuwa wanaishi utumwani Babeli wakati huu unabii ulionyeshwa kwa Ezekieli. Baada ya miaka 70 utumwani, Wayahudi walirudi kwa nchi yao. Lakini waliendelea kutawaliwa na mataifa mengine.

Wakati wa utawala wa Warumi, yaani baada ya Wayahudi kusulibisha Bwana Yesu Kristo, Warumi waliharibu Yerusalem. Mwaka wa 70 baada ya Yesu Wayahudi walivurushwa kutoka kwa nchi yao na kutawanyika kwa dunia yote. Wayahudi hawakuishi kama taifa moja tena.

Maono ya Ezekieli, aliona kwa bonde mifupa iliyokufa imetawanyika. Mifupa ilikuwa kavu sana. Hakukuwa na tumaini kwamba hiyo mifupa inaweza kuwa hai tena. Hii ilikuwa kama taifa la Israeli (Wayahudi) baada ya kutawanyika mwaka wa 70 baada ya Yesu. Hawakuwa taifa tena.



Bonde ililoja mifupa mikavu

Wayahudi walitawanyika kwa nchi zote za dunia. Taifa lilikufa na kutawanyika kama mifupa. Ilionekana kwamba hakutawezekana Wayahudi warudi kwa nchi yao na kuwa taifa tena.


Mungu aliambia Ezekieli ambie mifupa ikuje pamoja na kuungana. Ezekieli aliona mifupa ikija pamoja na kuungana na kujaa hilo bonde. Ezekieli aliambia nyama zikuje kwa mifupa na kukawa hivyo na sasa bonde lilijaa miili. Lakini hakukuwa na uhai kwa hizo miili. Ezekieli aliambia upepo uvume juu ya hizo miili na ipulize hewa ndani yao halafu iwe hai. Upепо ulivuma na hizo miili zikawa hai na zikasimama – jeshi kubwa.

Ezekieli 37:11 – 12 inaeleza maana ya huu unabii. Mungu anawambia watu wake, Wayahudi kwamba watatoka kwa nchi zingine kwenye aliwatawanyisha na kuwarudisha. Itakuwa kama taifa linatoka kaburini. Taifa litaishi tena na Mungu atawarudisha kwa nchi yao.

Unabii huu ultimizwa juzijuzi. Karibu miaka elfu mbili Wayahudi walikuwa wametawanyika katika nchi zingine duniani kote. Katika historia ya juzijuzi Mungu amekuwa akitimiza unabii aliompa Ezekieli miaka mingi iliyopita. Wakati wa Vita vya Pili vya Dunia, Mjeremani Nazi aliteza Wayahudi. Hitler aliamrisha mamilioni ya Wayahudi wauawee. Baada ya vita, watu walisikitia matezo ya Wayahudi. Wayahudi walipewa nchi ya Israeli kama yao. Mwaka wa 1948, Wayahudi walikuwa taifa tena kwa nchi yao. Maelfu ya Wayahudi walirudi kuishi kwao. Sasa hivi Israeli ni taifa, wanaishi na jeshi la nguvu.

Unabii huu uliongelea mambo yatakayokuwa kwa ulimwengu. Mataifa yote yenye Danieli alisema yalitawala Mashariki ya Kati kama vile Mungu alisema kwa Danieli. Watu wa taifa la Israeli walitawanyika dunia nzima lakini sasa ni taifa la nguvu kwa nchi yao sasawa na vile Mungu alisema kwa Ezekieli.

Tena Mungu atatimiza mwisho wa huo unabii. Hivi karibuni Bwana Yesu Kristo atakuja kama hilo jiwe. Ataharibu mataifa yote na kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani. Atatawala ulimwengu mzima kutoka Yerusuamu.



Miili ilisimama - jeshi kubwa